



1.je! sanduku la agano lilitengenezewa kwa mbao za mti gani?

2.je katika Israeli ni kabilia gani ambalo Mungu aliliondoa katika kitabu cha ufunuo kwa sababu ya uovu wao na kuwapa nafasi hiyo wana wa Yusufu?

3.Je katika biblia ni nani aliye weka nadhiri ya kuwa akishinda vita ananapo ludi nyumbani wakwanza kumlaki itakuwa sadaka ya Kuteketezwa kwa Bwana na akatoka binti yake?

4. A) Je! Ni mfalme gani aliye tawala Israeli kwa muda mchache kuliko wote?

B)je! ni mfalme gani aliye tawala yuda kwa muda mrefu zaidi kuliko wote?

5.je YESHURUNI ni nani?

6. Je! Paulo baada tu ya kuokoka alienda mji gani?

7.je andiko hili lapatikana wapi katika biblia (mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume)?

8.je ni mji gani ambako Bwana Yesu aligeuza Maji kuwa divai?

9. Taja tofauti za imani zinazo watofautisha mafarisayo na masadukayo?



10.je ni mji gani katika biblia ambao Bwana Mungu aliuteketeza kwa moto?

Mtihani mwema mjoli wa Bwana.

@NURU YA UPENDO
www.wingulamashahidi.org
0652274252 au 0693036618

26/02/2023

MAJIBU YA MTIHANI LEO

MTIHANI WA BIBLIA (PART 10)
(MASWALI YA BIBLIA)

1.je! sanduku la agano lilitengenezewa kwa mbao za mti gani?

Jibu. MTI WA MSHITA
Soma. Kutoka 25:10

2.je katika Israeli ni kabilia gani ambalo Mungu aliliondoa katika kitabu cha ufunuo kwa sababu ya uovu wao na kuwapa nafasi hiyo wana wa Yusufu?



Jibu. Kabilia la DANI

Soma .ufunuo 7:4-8

Sababu ya Mungu kuliondoa kabilia hilo ni.

==Ndio kabilia la kwanza kuleta miungu mingine katika Israeli walipo fika katika nchi ya kaanani.

Soma waamuzi 18:1-31

3.Je katika biblia ni nani aliye weka nadhiri ya kuwa akishinda vita ananapo ludi nyumbani wakwanza kumlaki itakuwa sadaka ya Kuteketezwa kwa Bwana na akatoka binti yake?

Jibu. YEFTHA

Soma. 11:34-40

4. A) Je! Ni mfalme gani aliye tawala Israeli kwa muda mchache kuliko wote?

Jibu. ZIMRI (siku 7)

Soma. 1Wafalme16:9-20

B)je! ni mfalme gani aliye tawala yuda kwa muda mrefu zaidi kuliko wote?

Jibu. MANASE (miaka 55)

Soma. 2Wafalme 21:1-18

5.je YESHURUNI ni nani?

Jibu. TAIFA LA ISRAELI

Soma. Isaya 44:1-2



6. Je! Paulo baada tu ya kuokoka alienda mji gani?

Jibu. ARABUNI

Soma. Wagalatia 1:13-18

7.je andiko hili lapatikana wapi katika biblia (mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume)?

Jibu. Kumbukumbu la torati 22:5

8.je ni mji gani ambako Bwana Yesu aligeuza Maji kuwa divai?

Jibu. Kana ya Galilaya

Soma. Yohana 2:1-12

9. Taja tofauti za imani zinazo watofautisha mafarisayo na masadukayo?

Jibu. Mafarisayo wana amini yote.

Masadukayo

i)Hawa amini ufufuo wa wafu

ii)Hawa amini kuwa kuna malaika

iii) hawa amini roho (roho ya mtu kuishi baada ya kufa,)

Soma. Matendo ya mitume 23:6-8

10.je ni mji gani katika biblia ambao Bwana Mungu aliuteketeza kwa moto?

Jibu. SODOMA NA GOMORA

Soma. Yuda 1:7

BWANA YESU awabariki sana.



26/02/2023 MTIHANI WA BIBLIA (PART 10) (MASWALI YA BIBLIA)

@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618